JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFIS YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI

Mkuu wa Shule ……………..0755668250
Makamu mkuuwa Shule…....0762125047
Patron:0769300255

Shule ya Sekondari Matema Beach,
S.L.P 122,
KYELA.
………………,

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi………..…………………………………………

S.L.P…………………………………...

…………………………………………

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATEMA BEACH HALMASHAURI YA KYELA MKOA WA MBEYA MWAKA ……………………..

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule ya sekondari hii mwaka ……………… na atasoma tahasusi ya …………..

Shule ya Sekondari Matema Beach ipo umbali wa Kilometa 38 Kaskazini mwa Mji wa Kyela. Usafiri wa basi kutoka mjini Kyela unapatikana katika kituo cha mabasi Kyela Nauli ni Shilingi 3,000 kwa basi.

Muhula wa masomo unaanza tarehe ......................... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuriport shuleni tarehe ................................ Mwisho wa kuriport ni tarehe ............................

2. Mambo muhimu ya kuzingatia;

2.1 Sare za shule

i) Sare ya shule ni suruali mbili; (Nyeusi na zambarau)

Suruali ishonwe kwa kawaida kabisa yenye mzunguko usiopungua inchi 14 miguuni kwa chini. Pia iwe na marinda ya mbele SIYO mitindo mingine ya kubana kama vile (MODO);

ii) Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu;
iii) Sare ya Michezo ni Viatu vya michezo, track suit na jezi ya blue jozi moja;
iv) Viatu vya shule ni Vyeusi vya kufunga kamba vyenye visigino vifupi;
v) Soksi jozi mbili Nyeusi za shule;
vii) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii) Sweta nyeusi yenye shingo V;
viii) Nguo za kushindia (shamba dress) ni suruali ya rangi ya khaki;
ix) Tai mbili, moja nyeusi na nyingine ya zambarau;
x) Tisheti (T-shirt) aina ya form six (inapatikana shuleni);

2.2 Mahitaji mengine ambayo mwanafunzi anapasawa kuja nayo shuleni;
i) Madaftari makubwa angalau quire 3 counter books dazani moja ;
ii) REAM (A4) ya karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv) Scientific Calculator kwa wanaosoma hisabati na jiografia;
v) Godoro lenye urefu wa futi 6, upana futi 2.5 na unene angalau inchi
3.5 vi) Mashuka Jozi 2 rangi ya pink , foronya ya godoro 1, chandarua 1;
vii) Nguo za ndani za kutosha;
viii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe );
ix) Ndoo 2 ndogo (lita kumi) au moja ya lita 20; zenye mifuniko;
x) Kwanja 1, jembe 1, mfagio wa ndani 1 na rubber drier 1

2.3 Michango

mbalimbali a) Shule

za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

MUHIMU:

- Shilingi 80,000/= (Elfu Themanini tu) ilipwe kwenye akaunti ya shule namba 60901200054. Jina la akaunti ni Matema Beach Sekondary School.

- BIMA YA AFYA
  Ikiwa hana bima ya afya, aje na Tsh 50,400/= (Hamsini elfu mia nne tu) ataandikishwa mfuko wa taifa wa bima ya afya.

## 3. Sheria na kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini . Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuriport shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

3.1 Sheria na kanuni za Shule

i) Heshima kwa viongozi ,wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku ( Preparation).
iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule na mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi) Kutunza usafi wa mwili , mavazi na mazingira ya shule.
vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix) Kutunza mali za shule.
x) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari na
xi) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya wmanafunzi
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa mkuu wa shule. ( Msiba au Ugonjwa).

3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule nipamoja na:
i) Wizi
ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro
iii) Kugombana na kuhamasisha ugomvi
iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu na jamii kwa ujumla.
v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule;
vi) Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii) kufuga ndevu
viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
ix) Uvutaji wa sigara
x) Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa ua kuolewa
xi) kusababisha mimba
xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xiii) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni
xiv) Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xv) Kudharau Bendera ya Taifa

xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu. Na
xvii) Uharibifu wa mali ya umma kwa maksudi.

**4. Viambatanisho na Fomu Muhimu**

i) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali.
ii) Fomu ya Maelekzo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.
iv) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa wanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamlifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……………………………

SOLOMON A. MWAIPOPO
MKUU WA SHULE

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao) Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZA SIMU ZILIZOORODHESHWA HAPO JUU.

FORM A

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**( THIS FORM IS TO BE COMPLETED BY A MEDICAL OFFICER)**

Name of pupil ……………………………………………… Age ……… Sex ……. The above named has been examined in respect of

a) STOOL …………………………………………………..

b) URINE …………………………………………………...

c) CHEST …………………………………………………..

d) BLOOD …………………………………………………

e) EYES …………………………………………………..

f) EARS ……………………………………………………

g) OTHER FINDINGS ………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………...

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

I am satisfied that the above named pupil is not fit to pursue further studies in any secondary school.

| | |
|---|---|
| …………………. | …………………….. |
| SIGNATURE | DATE |
| ………………… | …………………………... |
| DESIGNATION | STATION |

FOMU B

MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

(IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE)

Mimi (taja jina lako kamili) ……………………………………………………. nimechaguliwa kujiunga na masomo ya Elimu ya Sekondari kidato cha V 2023 katika shule ya Sekondari Matema Beach. Najaza fomu hii kukubali kuchaguliwa kwangu kuendelea na masomo katika shule hii. Naahidi kuwa niwapo katika shule hii nitatii na kufuata sheria na kanuni zote za shule kwa kipindi chote cha masomo yangu.

Pia na ahidi kuwa muda niwapo katika shule hii sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Kama nitakiuka na kwenda tofauti na mkataba huu, naomba sheria kali zichukuliwe dhidi yangu yaani kufukuzwa shule na kushtakiwa Mahakamani. Nakubali kuwa nitatekeleza na kufuata sheria na kanuni zote za shule.

SAHIHI YA MWANAFUNZI ……………………………..

TAREHE ……………………………..

FOMU C

FOMU YA MZAZI/ MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, KULIPA ADA, MICHANGO NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

(IJAZWE NA MZAZI/MLEZI MWENYEWE)

Mimi mazazi/Mlezi (Jina kamili) ……………………………………………….. Ambaye ni Mzazi/Mlezi wa (Jina kamili la Mwanafunzi) ………………………………………………… najaza fomu hii kukubali maelezo yaliyoandikwa hapo juu. kwa kujaza fomu hii. Naahidi kuwa nitatekeleza kwa vitendo katika kuhakikisha kuwa mwanafunzi huyu anapata mahitaji yote (yake binafsi na mahitaji ya Shule) kwa muda wote wa masomo ya Elimu ya Sekondari akiwa Matema Beach Sekondari.

Iwapo sitatimiza wajibu wangu, naahidi kuwa sheria zichukuliwe dhidi yangu.

SAHII YA MZAZI/MLEZI ………………………

TAREHE ………………………

FOMU D

HABARI KUHUSU MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi (Jina hilo ndilo litakalotumika siku zote bila kubadilika)

……………………………………………………………………………….

2. Tarehe ya kuzaliwa …………………………………………………

3. Mahali alipozaliwa (Wilaya) …………………………………………

4. Mahali anapoishi sasa (Wilaya) ………………………………………

5. Jina la Baba/Mlezi…………………………………………………

6. Anuani ya Baba /Mlezi …………………………………………….

7. Namba ya simu …………………………………………………...

8. Jina la Mama /Mlezi ………………………………………………...

9. Dini ya Mwanafunzi ………………………………………………..

10. Dini ya Baba /Mlezi ……………………………………………….

11. Dini ya Mama/Mlezi ………………………………………………

12. Kazi ya Baba/ Mlezi ………………………………………………

13. Michezo atakayoshiriki shuleni ni ………………………………..

FOMU E

MKATABA WA KUDHIBITI MAJANGA YA MOTO NA MATUMIZI YA SIMU KWA WANAFUNZI

(IJAZWE NA MWANAFUNZI PAMOJA NA MZAZI)

Mimi (taja jina lako kamili) ……………………………………………………………. nimechaguliwa kujiunga /mwanafunzi wa kidato cha …………… mwaka ………….

Ninaahidi kuwa niwapo katika shule hii sitatumia au kumiliki simu. Kama nitakiuka au kwenda kinyume na mkataba huu nitakuwa tayari kuadhibiwa na sheria ya shule inaopiga marufuku matumizi ya simu na adhabu yake ni kufukuzwa shule au kilpia fidia isiyopungua 800,000/= ( Laki nane tu) kwa kosa la matumizi ya simu na kuhatarisha usalama. Endapo Adhabu hiyo inaweza kuongezeka au sheria ya makosa ya jina kutumika.

SAHIHI YA MWANAFUNZI TAREHE

………………………………. ……………………..

Mimi ………………………………………………… ambaye ni mzazi / Mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa katika mkataba huu nimesoma na kuelewa na nitakuwa tayari kuwajibishwa kulingana na mkataba huu

SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI ……………….. TAREHE ……………...

SIMU YA MZAZI/MLEZI …………………….